**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

# MWONGOZO WA UTAMBUZI, USAJILI NA UFUATILIAJI WA MIFUGO







**UMETOLEWA NA**

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

**Toleo la Pili** **NOVEMBA, 2022**

## YALIYOMO


**1.0 UTANGULIZI** .... 1

**2.0 MALENGO YA MWONGOZO** .... 4

**2.1. Lengo Kuu la Mwongozo** .... 4

**2.2. Malengo Mahsusi ya Mwongozo** .... 4

**3.0 FAIDA NA UMUHIMU WA ZOEZI LA UTAMBUZI, USAJILI NA UFUATILIAJI WA MIFUGO** .... 4

**4.0 UTARATIBU WA UPATIKANAJI, BEI ELEKEZI NA GHARAMA ZA UWEKAJI HERENI UWANDANI** .... 5

**4.1. Upatikanaji wa hereni** .... 6

**4.2. Bei ya hereni za utambuzi na gharama za uwandani** .... 6

**4.2.1. Bei ya hereni** .... 6

**4.2.2. Gharama za Uvalishaji wa Hereni Uwandani** .... Error! Bookmark not defined.

**4.3. Uratibu wa mazoezi mengine ya utambuzi yaliyofanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi (ADGG/PAID)** .... 6

**5.0 MAJUKUMU YA WADAU WAKATI WA ZOEZI LA UWEKAJI WA ALAMA ZA UTAMBUZI KWA MIFUGO** .... 7

**5.1. Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Sekta ya Mifugo** .... 7

**5.2. Majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI** .... 8

**5.3. Majukumu ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa** .... 8

**5.4. Majukumu ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya** .... 9

**5.5. Ofisi za Kanda za Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo (ZVCs)** .... 9

**5.6. Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM)** .... 10

**5.7. Majukumu ya Afisa Utambuzi wa Halmashauri** .... 11

**5.8. Chama cha Wafugaji Tanzania** .... 12

**5.9. Watoa Huduma Binafsi** .... 12

**5.10. Majukumu ya Serikali ya Kijiji au Mtaa** .... 13

**5.11. Majukumu ya Mzalishaji na Msambazaji wa Vifaa vya Utambuzi** .... 14

**5.12. Majukumu ya Mfugaji** .... 15

**6.0 KUTOA NA KUHAMISHA UMILIKI WA MIFUGO KWENYE MFUMO WA UTAMBUZI** 15

**7.0 UTEKELEZAJI WA MWONGOZO HUU** .... 16

**8.0 HITIMISHO** .... 16

DIBAJI

Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo ni takwa la kisheria kama ilivyoanishwa kwenye Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mifugo ya Mwaka 2006, Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Na. 12 ya mwaka 2010 na Kanuni zake za mwaka 2011 pamoja na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020-2025. Pia, zoezi la utambuzi, usajili na Ufuatiliaji wa mifugo limeanishwa kwenye Sura Na. 4 na 5 ya viwango vya Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE standards, Chapters 4 and 5 for animals and animal products intended for export).

Tangu Kutoka kutungwa kwa Sheria ya Utambuzi na Usajili wa Mifugo, Wizara imekuwa na vipindi tofauti vya kuendesha zoezi la utambuzi na usajili wa mifugo. Kuanzia mwaka 2014 hadi 2017; wizara iliendesha zoezi la upigaji wa chapa za moto kwa ng'ombe zaidi ya milioni 17 walipigwa chapa. Mafanikio yalikuwa kidogo kutokana na changamoto kadhaa ikiwemo utunzaji hafifu wa kumbukumbu za mifugo iliyowekwa alama, kufutika kwa alama na kuharibu ubora wa ngozi kutokana na vidonda. Zoezi jingine lilikuwa la mwaka 2019 na 2020, ambapo njia ya kuweka hereni za kawaida hasa kwa ng'ombe wa maziwa iliendeshwa kwa gharama ya Shilingi 5,000= kwa kila ng'ombe bila kujumuisha gharama za uvishaji hereni. Zoezi hili pia lilikwama kutokana na wafugaji wengi kulalamikia bei kubwa ya zoezi.

Kutokana na changamoto zilizojitokeza kwenye mazoezi ya awali, Wizara ilifanya tathmini na kubaini njia ya kisasa ya kutambua na kusajili mifugo kwa kutumia hereni za kielektroniki zenye *barcode.* Njia hii haina madhara kwa mifugo ina ubora na ambayo mfugaji anaweza kumudu gharama yake. Aidha, Wizara ilitengeneza mfumo mzuri wa kielektroniki wa usajili na ambao unawezesha ufuatiliaji (traceability) kwa urahisi na unaokubalika kimataifa.

Katika kuhakikisha zoezi la Utambuzi na Usajili linatekelezwa kwa ufanisi, Wizara ilitengeneza toleo la kwanza la mwongozo wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo wa mwaka 2021 uliosainiwa tarehe 01/10/2021 unaotoa dira ya utekelezaji wa utambuzi wa mifugo kwa njia ya kielektroniki. Kupitia mwongozo huo, Wizara ilipanga kutambua na kusajili ng'ombe millioni 33.9, mbuzi millioni 24.5, kondoo millioni 8.5 na punda 657,389 kabla ya tarehe 31 Oktoba, 2022 kwa kutumia hereni za kielektroniki. Zoezi hili lilipangwa Kwenda sambamba na uingizwaji wa taarifa

kwenye mfumo maalum ambao unawezesha kuwa na kumbukumbu sahihi zinazoonesha aina ya mifugo, idadi, mmiliki, mahali alipo na taarifa nyingine muhimu zinazohusu mifugo. Hadi kufikia tarehe 31 Oktoba, 2022; jumla ya Mifugo **5,068,617** imetambuliwa na kusajiliwa kwenye mfumo ambayo ni sawa na **11%** ya lengo la kuweka alama za utambuzi kwa mifugo **45,920,000.**

Kutokana na kutofikiwa kwa malengo Wizara imepitia upya Mwongozo na kufanya maboresho kwenye masuala ambayo yamechangia kupatikana kwa mafanikio madogo katika zoezi lililotangulia. Toleo la pili la Mwongozo wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo unatoa suluhisho na kuendelea kutoa unafuu kwa Wafugaji wote nchini ikiwemo unafuu wa gharama za uwekaji wa hereni ambao utakuwa Shilingi 1,600 badala ya Shilingi 1,750/= kwa Ng'ombe na Punda na Shilingi 900/= kwa mbuzi na kondoo badala ya Shilingi 1,000/=. Vilevile, Mwongozo huu wa toleo la pili umeongeza ushirikishwaji wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya.

Aidha, mwongozo huu pia umeainisha utaratibu utakaotumika kuweka hereni kwa mifugo yote iliyokusudiwa katika Mikoa na Halmashauri zote nchini pamoja na utekelezaji wake ili kuboresha huduma ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo.

Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki (Mb)
**Waziri wa Mifugo na Uvuvi,**
**Novemba, 2022**

**1.0 UTANGULIZI**

Tanzania ni nchi ya pili kwa idadi ya ng’ombe barani Afrika, ikiwa na ng’ombe milioni 35.3. Mifugo mingine iliyopo nchini ni pamoja na mbuzi milioni 25.6, kondoo milioni 8.8 na punda 657,389, kuku milioni 92.8. Sekta ya mifugo inachangia asilimia saba (7.0%) katika pato la Taifa na asilimia ishirini na saba (27%) ya Pato la Sekta ya Kilimo ambapo asilimia arobaini (40%) ya pato hilo inatokana na uzalishaji wa nyama ya ng'ombe, asilimia thelathini (30%) inatokana na tasnia ya maziwa na asilimia thelathini (30%) inatokana na uzalishaji mbuzi, kondoo na kuku.

Katika kutekeleza takwa la kisheria, mahitaji ya sokomla kimataifa pamoja na kupata faida zingine nyingi za kuitambua na kuisajili mifugo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo) imepanga kutambua na kuisajili mifugo aina ya ng’ombe, mbuzi, kondoo na punda, ili kuweza kuboresha huduma za mifugo nchini kwa kufanya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo wa kupata idadi halisi ya mifugo iliyopo na namna bora ya kuboresha huduma za mifugo nchini. Kuitambua na kuisajili mifugo kutasaidia katika kutambua umiliki wa mifugo yote, kukabiliana na magonjwa ya mlipuko, kuwa na hakikisho la usalama wa chakula, kurahisisha biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi, udhibiti wa wizi wa mifugo, na kuwezesha upatikanaji wa mikopo na bima ya mifugo.

Zoezi la utambuzi, usajili na Ufuatiliaji ulianza mwaka 2014 mpaka 2017 ambapo ng’ombe zaidi ya milioni 17 walipigwa chapa ya moto na kanzidata ya TANLITS ilitumika kuweka kumbukumbu za utambuzi ili kuwezesha au kurahisisha ufuatiliaji wa mifugo (traceability). Upigaji chapa kwa mihuri ya moto ng’ombe uligubikwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na utunzaji hafifu wa kumbukumbu za mifugo iliyowekwa alama, kufutika kwa alama na kuharibu ubora wa ngozi kutokana na vidonda. Utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo kwa njia ya chapa pia ulikwama kutokana na kukosekana kwa mfumo mzuri wa kitaifa, uduni wa miundombinu na vifaa vilivyotumika ilisababisha kushindwa kufuatilia mifugo iliyotambuliwa kwa chapa na kutokidhi viwango vya kimataifa vya kibiashara.

Kati ya mwaka 2019 na 2020, Wizara ilianza utambuzi wa mifugo kwa njia ya kuweka hereni za kawaida hasa kwa ng’ombe wa maziwa, zoezi ambalo pia halikufanikiwa

kutokana na changamoto ya bei kuwa kubwa. Mfano katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara iliingia mkataba (zabuni) na kampuni ya Bajuta International na Mbabana General Agrovet wa kuagiza na kusambaza jumla ya hereni 500,000 kwa bei ya shilingi 5,000= kwa kila hereni bila kuwepo kwa gharama ya kuvisha hereni kwenye ng’ombe. Zoezi hili lilikwama pia kutokana na wafugaji wengi kulalamikia bei kubwa ya hereni na gharama za kuiweka kwa mnyama.

Kutokana na changamoto zilizojitokeza kwenye mazoezi ya awali ya utambuzi, Wizara ilifanya tathmini na kubaini mapungufu yaliyoambatana na zoezi kuweka alama za utambuzi kwa moto; kuharibika kwa ngozi na ni kinyume cha haki za wanyama. Hivyo, Wizara ilisitisha utambuzi wa mifugo kwa njia ya chapa na kubuni njia ya kutambua mifugo kwa kutumia hereni za kielektroniki zenye *barcode* pamoja na kutafuta njia ya kisasa ya utambuzi kwa njia ya hereni ambayo haina madhara kwa mifugo, yenye ubora mzuri na ambayo mfugaji anaweza kumudu gharama yake. Vilevile, kutengeneza mfumo mzuri wa kielektroniki wa usajili na ambao utawezesha ufuatiliaji (traceability) kwa urahisi na unaokubalika kimataifa.

Katika kuhakikisha zoezi la utambuzi na usajili linatekelezwa kwa ufanisi, Wizara ilitengeneza toleo la kwanza la Mwongozo wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo wa mwaka 2021 uliosainiwa tarehe 01/10/2021 na ambao ulitoa dira ya utekelezaji wa utambuzi wa mifugo kwa njia ya kielektroniki. Mwongozo huu uliandaliwa na kuhakikiwa na wadau zaidi ya 98 wa mifugo wakiwemo kutoka Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi, Makampuni yanaojishughulisha na kazi za mifugo, Chama cha Wafugaji Tanzania na Taasisi za Serikali na Wataalamu wastaafu.

Mwongozo toleo la kwanza uliainisha majukumu ya kila mdau anayehusika na utambuzi wa Mifugo kuanzia Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi, Msambazaji wa hereni, mfugaji, ofisi za Kanda, na Chama cha Wafugaji Tanzania. Kupitia mwongozo huu bei elekezi ya iliyopendekezwa kulipwa na mfugaji ni Shilingi 1,750= kwa uwekaji wa hereni kwa ng’ombe na punda na shilingi 1000= kwa mbuzi na kondoo. Bei hizi ziliandaliwa kwa kuzingatia gharama za uzalishaji

(laser beamed technology), uimara wa hereni husika na kwa kuzingatia gharama za uvalishaji wa hereni uwandani.

Katika utekelezaji wa toleo la kwanza la Mwongozo wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo wa mwaka 2021 yalijitokeza mapungufu katika utekelezaji wake yakiwemo namna ilivyopatikana gharama za hereni, kutokuainishwa baadhi ya majukumu ya wadau (Kamati ya ulinzi na Usalama ya Wilaya, Afisa Utambuzi wa Wilaya, Vyama vya wafugaji na Taasisi za Serikali na Binafsi); kutokutambuliwa kwa mazoezi mengine ya utambuzi yaliyofanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi (ADGG/PAID) na kutokuwepo kwa mchakato wa uagizaji wa hereni kutoka kwa mzalishaji.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi baada ya kubaini mapungufu yaliyojitokeza kwenye mwongozo toleo la kwanza imeandaa toleo la pili la Mwongozo wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo Novemba, 2022 ambao umeainisha na kuchanganua maeneo yafuatayo:

(i) Malengo ya mwongozo;
(ii) Utaratibu wa upatikanaji wa hereni, bei elekezi na gharama uwekaji hereni uwandani;
(iii) Usimamizi wa fedha zitakazotokana na zoezi la utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo;
(iv) Majukumu ya wadau wote wanaohusika na zoezi la utambuzi na usajili na ufuatiliaji wa mifugo;
(v) Matumizi ya mfumo wa TEHAMA wa utambuzi, uchukuaji wa taarifa uwandani, ufuatiliaji wa takwimu za utambuzi na kuhamisha umiliki wa mifugo;
(vi) Utekelezaji wa Toleo la Pili la Mwongozo wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo;
(vii) Hatua za kisheria zitakazochukuliwa kwa atakeyekaidi utekelezaji wa mwongozo

## 2.0 MALENGO YA MWONGOZO

### 2.1. Lengo Kuu la Mwongozo

Kujenga uwezo, kuanisha utaratibu, usimamizi, majukumu, matumizi ya mfumo wa TEHAMA, na mapokezi ya fedha katika zoezi la Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo Tanzania.

### 2.2. Malengo Mahsusi ya Mwongozo

i. Kujenga uelewa miongoni mwa wadau, kuainisha faida na umuhimu wa zoezi la Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo nchini;
ii. Kuratibu upatikanaji wa hereni, bei elekezi na gharama uwekaji hereni uwandani, matumizi ya Mfumo wa TEHAMA pamoja na usimamizi wa fedha zitakazotokana na zoezi la utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo;
iii. Kuanisha majukumu na hatua za kisheria kwa wadau wote wanaohusika na zoezi la utambuzi na usajili na ufuatiliaji wa mifugo;

## 3.0 FAIDA NA UMUHIMU WA ZOEZI LA UTAMBUZI, USAJILI NA UFUATILIAJI WA MIFUGO

Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo ni takwa la kisheria kama lilivyoanishwa kwenye Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mifugo ya Mwaka 2006, Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Na. 12 ya mwaka 2010 na Kanuni zake za mwaka 2011 pamoja na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020-2025. Pia, zoezi la utambuzi, usajili na Ufuatiliaji wa mifugo limeanishwa kwenye sura na. 4 na 5 ya viwango vya shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE standards, Chapters 4 and 5 for animals and animal products intended for export).

Kwa Tanzania, zoezi la utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo limeboreshwa kwa kutumia hereni za kielekroniki ambapo usajili hufanywa kwenye mfumo maalum wa TEHAMA unaowezesha kuwa na kumbukumbu sahihi za aina, idadi ya mifugo, mtawanyiko wake nchini na taarifa nyingine muhimu zinazohusu mifugo. Faida za Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo ni pamoja na Mifugo kutambulika ilipo na umiliki wake; kukabiliana na magonjwa ya mlipuko; kuwa na hakikisho la usalama wa chakula; kuongeza thamani ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi; udhibiti wa wizi wa mifugo; kurahisisha uboreshaji wa koosaafu za mifugo na kuwezesha

upatikanaji wa mikopo na bima ya mifugo kwa Wafugaji. Kwa wadau ambao hawatazingatia zoezi hili la utambuzi na usajili wa Mifugo, watakuwa wamekikuka Sheria hii ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo mwaka 2010, kifungu cha 12 na 24.

## 4.0 UTARATIBU WA UPATIKANAJI, BEI ELEKEZI NA GHARAMA ZA UWEKAJI HERENI UWANDANI

Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika kutafuta njia bora ya utambuzi na usajili wa mifugo, ilipokea maombi ya makampuni mbalimbali yaliyoonesha nia ya kutengeneza na kusambaza hereni za kielektroniki nchini. Makampuni manne (4) yalionesha teknolojia bora, upatikanaji wa hereni na vifaa vya utambuzi kwa gharama ambayo mfugaji anaweza kuimudu. Pia, makampuni hayo yaliweza kuonesha uwezo wa kuzalisha na kusambaza hereni na vifaa vya kuweka hereni (ear tag applicators) kwa wafugaji kwa gharama nafuu.

Lengo ni kwa Serikali kubaki na jukumu la kusimamia Sheria, Kanuni, Miongozo na ubora wa utoaji wa huduma hiyo kwa ufanisi na kwa dhana ya mashirikiano ya Serikali na Sekta Binafsi (Public Private Partneship). Kampuni ya S & J Animal Tech ilikidhi vigezo ikiwemo kuwa na kiwanda cha uzalishaji wa hereni kilichopo Jijini Dar es Salaam. Vigezo ambavyo vilitumika kuwapitia kazi kampuni ya S & J Animal Tech kuzalisha hereni za utambuzi wa mifugo nchini ni pamoja na:

(i) Uwezo wa kuzalisha hereni za kieletroniki ndani ya nchi ili kulinda usiri wa taarifa za utambuzi (confidentiality) ambazo zinahifadhiwa kwenye barcode;

(ii) Kuwa tayari kushiriki kwenye uoneshaji wa jinsi alama za utambuzi zinavyotumika (demonstrations) na kutoa vifaa vya utambuzi vyenye ithibati ya kimataifa (ISO) na ambavyo haviathiriwi na hali ya hewa ya joto, jua, mvua, unyevunyevu au vumbi la mazingira ya wafugaji wa Tanzania; na

(iii) Kuwa na historia ya kufanya kazi ya utambuzi wa mifugo nchini au nje ya nchi.

Aidha, barcode inaendelea kuwa ni mali ya Serikali na haitatumika bila ya kibali cha Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

### 4.1. Upatikanaji wa hereni

Mamlaka za Serikali za Mitaa zitakuwa msimamizi mkuu katika upatikanaji na uvishaji wa hereni katika Mamlaka husika. Utaratibu wa upatikanaji wa hereni upo wa aina tatu;

**(i) Zoezi la utambuzi na usajili kufanywa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa (MSM)**

Mamlaka itatuma maombi ya hereni kwa Katibu Mkuu Mifugo, na Katibu Mkuu Mifugo (KMM) atawasilisha maombi hayo kwa Mtengenezaji wa hereni za utambuzi na Mkurugenzi wa Halmashauri atajulishwa kwa barua na barua pepe; aidha hereni zitawasilishwa kwa mwombaji ndani ya masaa 72;

**(ii) Mzabuni (Sekta binafsi)**

Mzabuni aliyepewa mkataba wa kufanya kazi ya utambuzi na Halmashauri kupitia Mkurugenzi wa Halmashauri atalazimika kuagiza hereni za utambuzi zitakazopokelewa na kusimamiwa na Halmashauri;

(iii) Kwa wafugaji walio kwenye vyama, vikundi na wafugaji wakubwa (wanenepeshaji) wenye mifugo zaidi ya 500 wanaweza kuagiza hereni kwa kuwasiliana na kutuma maombi Mkurugenzi wa Halamashauri na kisha Mkurugenzi kutuma maombi kwa Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi na hereni zitaagizwa na kuletwa MSM; aidha kazi ya kuvika hereni itasimamiwa na Wataalamu wa MSM.

### 4.2. Bei ya hereni za utambuzi na gharama za uwandani

#### 4.2.1. Bei ya hereni

i). Bei ya ununuzi wa hereni moja ya ng’ombe na punda toka kwa mzalishaji na gharama za uvalishaji mifugo ni Tsh. 1,600/=

ii). Bei ya ununuzi wa hereni moja ya mbuzi na kondoo toka kwa mzalishaji na gharama za kuvalisha mifugo ni Tsh. 900/=

### 4.3. Uratibu wa mazoezi mengine ya utambuzi yaliyofanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi (ADGG/PAID)

Wizara ya Mifugo na Uvuvi inatambua mazoezi mengine ya utambuzi yalifanyika kwa nyakati tofauti nchini ikiwemo mradi wa uboreshaji na uendelezaji mbari za ng’ombe

wa maziwa kama *African Dairy Genetic Gain* (ADGG) ulianzishwa mwaka 2016. Mradi huo ulikuwa ni wa miaka sita. Lengo la mradi huo ulikuwa ni kuwa na mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za mifugo (utambuzi wa ng'ombe kwa kujua uzazi na ubora wake), pili kuweza kurejesha mrejesho kwa wafugaji pale wanapokuwa na maswali au maoni na tatu ni kuipanga mifugo kulingana na ubora wake ili kuwasaidia wafugaji kupata mifugo sahihi yenye uwezo wa kutoa maziwa mengi. Mradi huo kwa hapa Tanzania unafanyika katika mikoa saba (7) na Halmashauri ishirini na nne (24). Wizara inazitambua hereni ambazo zimeshavalishwa kupitia mradi, lakini kwa Mifugo mpya ambayo haina hereni za utambuzi; lazima uzingatie mwongozo huu mpya wa Wizara wa Utambuzi na Usajili wa Mifugo.

## 5.0 MAJUKUMU YA WADAU WAKATI WA ZOEZI LA UWEKAJI WA ALAMA ZA UTAMBUZI KWA MIFUGO

### 5.1. Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Sekta ya Mifugo

(i) Kuratibu na kuhakikisha upatikanaji wa hereni za kielektroniki kwa ajili ya zoezi la utambuzi, usajili na ufuatiliaji kwa mujibu wa Sheria na kuzisambaza kwa wadau wote kwa wakati;

(ii) Kukusanya taarifa za uwekaji wa hereni za utambuzi kutoka kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa (Local Government Authorities) kulingana na mwongozo wa utambuzi, utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo;

(iii) Kuhakikisha zoezi la utambuzi wa mifugo unafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji Mifugo Sura 184 (Sheria Namba 12 ya Mwaka 2010) na Kanuni zake (GN No: 362 ya Oktoba 2011);

(iv) Kuhakikisha kuwa kuna usimamizi madhubuti katika kufikia malengo kusudiwa ya utambuzi na idadi yote wa mifugo iliyopo;

(v) Kusimamia usanifu na ujenzi wa mfumo wa Kitaifa wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo (Tanzania National Livestock Identification and Traceability System) ambao ulianza mwaka 2012;

(vi) Kuratibu uhamasishaji na ufuatiliaji wa zoezi zima la uwekaji wa hereni za kielektroniki, kuhakikisha wafugaji wamehamasishwa na kuelewa umuhimu wa utambuzi wa mifugo;

(vii) Kusimamia na kuandaa namba na idadi ya hereni kwa kila Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(viii) Kuanisha na kushirikiana na miradi ya Kitaifa iliyoweka alama za utambuzi na kubuni namna nzuri ya kuziingiza alama hizo kwenye mfumo wa utambuzi, usajili wa ufuatiliaji wa Mifugo;

(ix) Kuimarisha na kuufanya mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa Mifugo kuwa chanzo cha taarifa za utambuzi na usajili wa mifugo nchini (Primary source of identification and registration of data);

(x) Kuratibu na kusimamia uchakataji na matumizi ya taarifa na takwimu za zoezi la Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji.

**5.2. Majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI**

(i) Kuwa kiungo kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kufanikisha utekelezaji wa maelekezo yote yanayotolewa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhusu uwekaji wa hereni kwenye mifugo iliyopo kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini;

(ii) Kuratibu na kuzisimamia Tawala za Mikoa ili kuziwezesha Halmashauri kufanikisha zoezi la Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo;

(iii) Kutoa utaratibu na kuzielekeza Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga fedha kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato ili kufanya zoezi la utambuzi na usajili wa mifugo kuwa endelevu;

(iv) Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni zinazohusiana na Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo;

(v) Kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wadau wengine kwenye uhamasishaji wa utambuzi wa mifugo katika Mikoa;

(vi) Kuratibu, kushauri, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa zoezi la utambuzi wa mifugo;

**5.3. Majukumu ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa**

(i) Ofisi za Wakuu wa Mikoa zitakuwa na jukumu la kushiriki katika kuhakikisha zoezi la utambuzi wa mifugo linafanikiwa katika Halmashauri zote ndani ya mkoa husika;

(ii) Kuzisimamia na kuhakikisha Halmashauri zote ndani Mkoa husika zinatambua na kusajili mifugo yote kusudiwa;

(iii) Kushiriki, kutoa elimu na kuhamasisha wadau; wafugaji, wafanyabiashara kwa kushirikiana na Wizara, Chama cha Wafugaji na Halmashauri kuhusu umuhimu wa zoezi la utambuzi wa mifugo;

(iv) Kushauri na kusimamia uendelevu wa zoezi la utambuzi na usajili wa mifugo wakati wowote ili kufanikisha zoezi;

(v) Kuhakikisha vifaa vya utambuzi vinafika katika Halmashauri husika ndani ya Mkoa kwa wakati;

(vi) Kuwa kiungo kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, OR-TAMISEMI na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika usimamizi, utekelezaji na ufuatiliaji wa zoezi la uwekaji alama za utambuzi na usajili wa mifugo.

**5.4. Majukumu ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya**

(i) Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya itasimamia utekelezaji wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo ya mwaka 2010 na Kanuni zake za Mwaka 2011 ndani ya Wilaya husika;

(ii) Kudhibiti na kusimamia hali ya Usalama, amani na utulivu katika maeneo yote ya zoezi la utambuzi ndani ya Wilaya;

(iii) Kuhakikisha usalama wa wataalam na viongozi wote wanaoshiriki zoezi la uhamasishaji, utambuzi na usajili katika Wilaya.

(iv) Kushauri namna bora ya kufanya kwa amani na usalama mazoezi ya uhamasishaji, utambuzi na usajili wa mifugo wakati wowote ili kufanikisha zoezi;

(v) Kuhamasisha zoezi la utambuzi na usajili wa Mifugo katika Wilaya husika.

**5.5. Ofisi za Kanda za Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo (ZVCs)**

(i) Kusimamia utekelezaji na kutoa ufafanuzi wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo ya mwaka 2010;

(ii) Kuhamasisha na kufuatilia zoezi la usajili na utambuzi kwenye Halmashauri zote husika kwa kushirikiana na Wadau wengine waliopo kwenye kanda husika;

(iii) Kuratibu ukusanyaji wa taarifa za idadi ya mifugo iliyowekewa alama za utambuzi na kuhakikisha zinaingizwa kwenye mfumo wa utambuzi kila siku;

(iv) Kuhakikisha zoezi la utambuzi na usajili wa mifugo linafanyika kwenye Halmashauri zote ndani ya Kanda pamoja na kuhakikisha alama za utambuzi zinawekwa kwenye mifugo yote;

(v) Kutoa taarifa ya mazoezi mengine ya utambuzi yaliyofanywa katika Kanda husika na kupendekeza namna ya kuyaunganisha mazoezi hayo.

**5.6. Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM)**

(i) Wakurugenzi wa Halmashauri wanapaswa kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo ya mwaka 2010 na Kanuni zake za Mwaka 2011;

(ii) Kutoa na kuwasilisha taarifa za idadi ya mifugo (Ng'ombe, Mbuzi, Kondoo na Punda) iliyopo kwenye Halmashauri husika na kuiwasilisha Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ajili kuandaa mahitaji ya hereni;

(iii) Kuingia makubaliano na mzalishaji na msambazaji wa hereni za utambuzi wa mifugo kwa njia za kielektroniki ili kuwa na utaratibu mzuri wa malipo;

(iv) Kuteua Afisa Utambuzi wa Mifugo ambaye majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye **kipengele cha 5.7** kinachoelezea Afisa Utambuzi wa Halmashauri**;**

(v) Kusimamia zoezi la uwekaji wa hereni za utambuzi kwa kutumia wataalam wa Halmashauri husika;

(vi) Kuingia mikataba na watoa huduma au makampuni binafsi kwa ajili ya kufanya zoezi la uwekaji wa hereni za utambuzi pamoja na kuingiza taarifa zake kwenye mfumo wa kitaifa la utambuzi na usajili wa mifugo;

(vii) Kuhakikisha taarifa zote za utambuzi za kila siku zinaingizwa kwenye mfumo wa Kitaifa wa utambuzi na usajili wa mifugo kwa kuwatumia Maafisa Utambuzi na TEHAMA wa Halmashauri;

(viii) Kuhamasisha wadau wote wa mifugo walioko kwenye Halmashauri husika kutambua mifugo yao kwa kutumia Hereni za Kielektroniki zinazotambuliwa na Serikali;

(ix) Kuhuisha na kuhakikisha taarifa za mifugo inayouzwa minadani, kuchinjwa, kufa au kutolewa mahari; zinabadilishwa umiliki wake kwenye mfumo wa utambuzi ndani ya siku 14. Kwa mifugo inayozaliwa, itatakiwa kutambuliwa na

kusajiliwa kuanzia umri wa siku moja hadi miezi mitatu (3) na kusajiliwa kwenye mfumo;

(x) Kutunza vifaa vya uwekaji wa hereni kwa mifugo kwa kila Kata ili kuwezesha uwekaji endelevu wa alama za utambuzi na usajili;

(xi) Vibali vyote vya kusafirisha mifugo ndani na nje ya nchi vitatolewa tu kwa mifugo iliyowekwa alama za utambuzi;

(xii) Kukusanya fedha za malipo na kutoa resiti za kielekroniki kwa wafugaji wanaopewa huduma za utambuzi wa mifugo yao;

(xiii) Kuhakikisha malipo ya fedha zote za hereni yanafanyika kabla mzalishaji na msambazaji wa hereni hajazipeleka kwenye Halmashauri yake kulingana na mahitaji ya wakati huo;

(xiv) Kusimamia na kuwezesha utekelezaji wa zoezi la utambuzi wa mifugo na kuhakikisha taarifa zote zinahifadhiwa kwenye mfumo.

**5.7. Majukumu ya Afisa Utambuzi wa Halmashauri**

(i) Afisa Utambuzi wa Halmashauri atasimamia utekelezaji wa shughuli zote za Utambuzi kwa mujibu wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo ya mwaka 2010 na Kanuni zake za Mwaka 2011;

(ii) Kutoa na kuwasilisha mahitaji ya hereni ya Halmashauri yake na kuziwasilisha kwa wakati kwa Mkurugenzi kwa ajili ya kutengenezewa hereni kutoka kwa mtengenezaji kila zinapohitajika;

(iii) Kusimamia zoezi la utambuzi litakapokuwa linafanyika mahali popote katika Halmashauri yake;

(iv) Kuhakikisha mifugo yote iliyopo katika Halmashauri inasajiliwa kwa mujibu wa Sheria za nchi, taratibu na kanuni zilizopo;

(v) Kukusanya na kutunza takwimu zote utambuzi zikiwepo za:

a. Idadi ya mifugo iliyotambuliwa
b. Idadi ya hereni zilizovalishwa kwa mifugo yote kila siku;
c. Idadi ya mifugo iliyozaliwa, iliyokufa, liyochinjwa, iliyonunuliwa, iliyouzwa popote na minadani, na kuhuisha tarifa zake kwa mujibu wa maelekezo ya Kanuni ya Utambuzi ya mwaka 2011;

(vi) Kuhuisha takwimu za mifugo iliyotambuliwa na kuingiza takwimu hizo kwenye mfumo wa utambuzi kila siku kwa mujibu wa Sheria, taratibu na Kanuni zilzopo zinavyoelekeza;

(vii) Kuhifadhi nyaraka zote na vifaa vya utambuzi katika Halmashauri na kuhakikisha vinakuwa salama

(viii) Kuratibu na kusimamia zoezi la utambuzi katika maeneo yote ya Halmashauri;

(ix) Kushirikisha taasisi na Vyama vingine kama vya Wafugaji katika zoezi lote la Uhamasishaji, utambuzi na usajili wa mifugo.

(x) Kuhakikisha zoezi la uhamasishaji, utambuzi na usajili linafanyika kwa kushirikisha vyombo vingine na taasisi binafsi kama wazabuni watakaokuwa wamepewa mikataba ya kuvisha hereni katika Halmashauri

(xi) Kutoa tarifa ya zoezi zima la utambuzi katika Halmashauri na kwa Afisa Utambuzi wa Wizara ya Mifugo kila wiki.

### 5.8. Chama cha Wafugaji Tanzania

(i) Kuhamasisha wafugaji kujitokeza kwa ajili ya kuweka alama za utambuzi wa mifugo katika maeneo yao;

(ii) Kuwahamasisha na kuwaelimisha viongozi wa wafugaji, wazee maarufu na wazee wa mila wa vijiji kutambua na kukubali zoezi la utambuzi wa mifugo na hatimaye kuwahamasisha kwa wafugaji wengine**;**

(iii) Kuwaunganisha Wafugaji kupitia vikundi kwa kushirikiana na Halmashauri ili waweze kunufaika na fursa zilizopo katika maeneo yao ili kufanikisha zoezi la utambuzi wa Mifugo.

### 5.9. Watoa Huduma Binafsi

(i) Kuhakikisha kuwa wamekidhi matakwa ya kisheria na kitaaluma ya utoaji wa huduma za afya za wanyama ikiwemo ya uwekaji wa alama za utambuzi kwa mifugo kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Veterinari ya mwaka 2003 kwa kuwa wamesajiliwa (Animal Health Services Company) na Baraza la Vaterinari la Tanzania (VCT);

(ii) Kuwasilisha maombi ya kazi ya kuweka hereni za kielektroniki kwa mifugo ya Halmashauri husika na pale atakapokubaliwa watawekeana mkataba wa

kufanya kazi hiyo kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji ya mwaka 2010 na Kanuni zake za Mwaka 2011;

(iii) Kutumia alama za utambuzi zilizokubaliwa na Serikali kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu;

(iv) Kuingia makubaliano na Halmashauri ili kuweza kushiriki kwenye zoezi la uwekaji wa alama za utambuzi na kusajili mifugo;

(v) Kushiriki katika maandalizi ya awali ya uwekaji wa alama za utambuzi yatakayoshirikisha vikao baina ya Halmashauri, Chama cha wafugaji na wadau wengine;

(vi) Kushirikiana na Halmashauri na wadau wengine wakati wa zoezi la uhamasishaji na ufuatiliaji wa ufanisi katika utoaji wa huduma ya uwekaji wa alama za utambuzi wa mifugo;

(vii) Makampuni yaliyopata kazi ya kuweka hereni za kielektroniki kwa mifugo kuhakikisha yanafuata taratibu zote zilizowekwa na Wizara ya Mifugo kuhusu uwekaji wa hereni za kielektroniki kwa mifugo.

**5.10. Majukumu ya Serikali ya Kijiji au Mtaa**

(i) Kuwahamasisha Wanachi na vikundi vya wafugaji ngazi ya viongozi juu ya umuhimu wa uwekaji wa alama za utambuzi wa wafugaji yote na kuhakikisha kila mfugaji anashiriki kikamilifu kwenye zoezi hili;

(ii) Kuandaa maeneo na miundombinu ya kutolea huduma za utambuzi na usajili ndani ya Mtaa au Kijiji husika;

(iii) Kuhakikisha mifugo yote kwenye Kijiji au Mtaa inawekwa alama za utambuzi;

(iv) Kutunza kumbukumbu za wafugaji ambao mifugo yao imetambuliwa na kusajiliwa na hiyo ndiyo itakuwa mifugo halali katika kijiji husika;

(v) Kutoa taarifa kwa Afisa Mifugo wa Kata, Kijiji, Mtaa au Wilaya pale ambapo kutakuwa na taarifa ya kuuzwa kwa mifugo, kutolewa mahari, kusafirishwa au kuchinjwa na;

(vi) Kutoa taarifa kwa Afisa Mifugo wa Kata au Wilaya pale inapotokea baadhi ya wafugaji wamekaidi kuweka alama za utambuzi kwa mifugo yao ili waweze kuchukuliwa hatua za kisheria.

### 5.11. Majukumu ya Mzalishaji na Msambazaji wa Vifaa vya Utambuzi

Mzalishaji na msambazaji ni mdau toka Sekta Binafsi aliyetambuliwa na kusajiliwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya kuzalisha na kusambaza hereni za kielektroniki pamoja na vifaa vya utambuzi wa mifugo Tanzania Bara. Ili kuwa na udhibiti kwenye kutoa namba za utambuzi, idadi ya hereni za utambuzi zinazozalishwa pamoja na kudhibiti ubora, Wizara imetoa zabuni kwa Mzalishaji mmoja tu ambaye amepewa alama maalum ya kielektroniki (barcode) ambayo ni mali ya Serikali na inawekwa kwenye hereni za utambuzi. Hereni za utambuzi zitazalishwa hapa nchini na kusambazwa kwenye Halmashauri kwa utaratibu unaoratibiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Majukumu ya Mzalishaji na Msambazaji wa vifaa vya utambuzi ni pamoja na:

(i) Kuhakikisha kuwa amekidhi matakwa ya kisheria na kitaaluma ya uzalishaji na usambazaji wa vifaa vya utambuzi wa mifugo kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Veterinari ya 2003 pamoja na kuwa wamesajiliwa na Baraza la Vaterinari la Tanzania;

(ii) Kuwa na kibali cha Wizara ya Mifugo na Uvuvi kufanya kazi hiyo;

(iii) Kutengeneza na kusambaza vifaa vya utambuzi wa mifugo vya kutosheleza mahitaji na vyenye ubora stahiki kwa wakati na kwa idadi inayotakiwa;

(iv) Kuzalisha vifaa vya utambuzi (hereni za kielekroniki) kulingana na mahitaji yaliyopo kwenye Halmashauri.

(v) Mzalishaji na Msambazaji hataruhusiwa kuzalisha hereni za kielektroniki zenye barcode ya Serikali na kuziuza kwenye maduka ya pembejeo za mifugo au kwingineko;

(vi) Kuuza vifaa vya utambuzi wa mifugo kwa Halmashauri au kwa watoa huduma za mifugo binafsi waliokidhi vigezo na ambao wataenda kuziweka kwa mifugo na sio kuziuza madukani;

(vii) Kuwasilisha kwa Wizara nakala ya orodha na namba za hereni za utambuzi zilizozalishwa na kusambazwa ili kuhakikisha kunakuwa na takwimu sahihi kwa kila Halmashauri iliyopelekewa hereni;

(viii) Kulipia gharama za usambazaji wa vifaa vya utambuzi wa mifugo katika ngazi ya makao makuu ya Halmashauri.

### 5.12. Majukumu ya Mfugaji

(i) Kuhakikisha kuwa ng'ombe, punda, mbuzi na kondoo wote anaowamiliki wamewekwa alama za utambuzi na wamesajiliwa kwenye mfumo na mtaalamu wa mifugo kutoka kwenye kijiji, Kata, Halmashauri au kampuni binafsi ya kutoa huduma za mifugo iliyopewa kazi hiyo na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(ii) Kushirikiana na viongozi wa chama cha wafugaji katika Kijiji au Mtaa, Kata na Wilaya katika shughuli zote zinazohusu uwekaji wa alama za utambuzi;

(iii) Kupeleka kwenye vituo vilivyoainishwa na kuhakikisha mifugo yake yote imewekwa alama za utambuzi za kielektroniki na inatambuliwa;

(iv) Kulipia gharama za ununuzi wa hereni za mifugo yote kwa bei elekezi isiyozidi shilingi 1,600/= kwa ng'ombe na punda na shilingi 900/= kwa mbuzi na kondoo.

(v) Kutoa taarifa ya mifugo ndani ya siku 14 kwa Afisa mifugo wa Kijiji au Kata kuhusu mifugo iliyokufa, iliyochinjwa, iliyouzwa, iliyonunuliwa na iliyotolewa mahari ili iweze kuondolewa au kuingizwa kwenye mfumo wa usajili;

(vi) Kutoa taarifa ya mifugo iliyopoteza hereni za utambuzi ndani ya siku 14 kwa Afisa mifugo wa kijiji au Kata ili kupatiwa hereni nyingine za utambuzi na kusajiliwa kwenye mfumo na;

(vii) Kutunza daftari la kumbukumbu ya namba za hereni za utambuzi zilizowekwa katika mifugo yake kwa lengo la kutunza taarifa za umiliki.

## 6.0 KUTOA NA KUHAMISHA UMILIKI WA MIFUGO KWENYE MFUMO WA UTAMBUZI

Katika kuhakikisha takwimu za mifugo iliyopo zinaakisi uhalisia wa idadi ya mifugo iliyopo mahali popote nchini, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeweka utaratibu wa kuhuisha takwimu zote za mifugo itakayozaliwa, itakayokufa, itakayouzwa, itakayochinjwa, au itakayotolewa kama zawadi, mahari ambapo umiliki wake utahamishwa kutoka kwa mmiliki wa awali na kuingizwa takwimu zake kwa mmiliki aliyehamishiwa kwa mujibu wa Sheria, Taratibu na Kanuni kama ifuatavyo:-

(i) Mifugo itakayochinjwa au kufa itaondolewa kwenye mfumo na Afisa Utambuzi mifugo wa Halmashauri wa eneo husika au Afisa yeyote atakayepewa jukumu hilo na mamlaka husika na kwa mujibu wa kanuni ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo ya mwaka 2011 (Livestock departure declaration form 10$^{th}$ schedule);

(ii) Mifugo itakayouzwa, kutolewa zawadi au mahari itahamishwa taarifa za umiliki wake kutoka mmiliki wa sasa kwenda ilikopokelewa; uhamisho huu utafanywa na Afisa Utambuzi mifugo wa Halmashauri wa eneo husika au Afisa yeyote atakayepewa jukumu hili (Livestock arrival Notification form eleventh schedule);

(iii) Mifugo inayohama kutoka Wilaya moja kwenda nyingine itapewa kibali cha kuhamisha mifugo au kusafirisha kwa kuzingatia sheria taratibu na miongozo uliopo kabla ya kusafirisha;

(iv) Mifugo yote itatakiwa kutambuliwa mara tu baada ya kuzaliwa na sio zaidi ya miezi mitatu.

## 7.0 UTEKELEZAJI WA MWONGOZO HUU

Mwongozo huu wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo utaanza kutumika rasmi tarehe 01/02/2023 hadi tarehe 30/06/2023. Hivyo, mdau yeyote atakayekuwa kinyume na mwongozo huu katika kutekeleza majukumu ya utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo atachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria na taratibu zilizopo.

## 8.0 HITIMISHO

(i) Mifugo yote ambayo haijatambuliwa (Ng'ombe, punda, kondoo na mbuzi) hawataruhusiwa kuuzwa minadani, kusafirishwa, kutolewa mahari au kuchinjwa machinjioni;

(ii) Mfugaji ambaye atakuwa hajaweka alama za utambuzi wa mifugo ataelimishwa zaidi na ifikapo 01/07/2023 atachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria**;**

(iii) Zoezi la uwekaji alama za utambuzi na usajili liende sanjari na Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Sekta Binafsi na Chama Cha Wafugaji kutengeneza mpango bora uboreshaji wa maeneo ya malisho na upatikanaji wa maji kwa mifugo maana idadi yake itakuwa inajulikana;

(iv) Mfugaji akishaitambua mifugo yake aelimishwe namna ya kuwekeza kwenye kuboresha koosafu na kupanga namna ya kupata malisho yatakayotosheleza mifugo yake kwa mwaka mzima.